# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

## HALMASHAURI YA WILAYA NACHINGWEA

SHULE YA SEKONDARI NAMBAMBO,
S.L.P 50
**NACHINGWEA**.

***KUMB. NA. NBB/S 2004/J/*** 07/12/2020

MZAZI/MLEZI WA …………………………………………… NA. YA MTIHANI…..........................……
C/O MWL. MKUU S/M ………………………………………..
S.L.P 49,
**NACHINGWEA**.

**YAH: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NAMBAMBO KIDATO CHA KWANZA -2019</u>**

**1.0. UTANGULIZI**

Kwa niaba ya uongozi na Jumuia ya sekondari ya Nambambo nachukua fursa hii kumpongeza mwanao kwa kuchaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Nambambo.

Shule ya sekondari Nambambo ipo km 1.4 kutoka barabara ya polisi kuelekea Voda. Ni shule ya mchanganiko ya kutwa.Shule inafundisha masomo tisa ya msingi kama ifuatavyo:- URAIA, HISTORIA, JIOGRAFIA, KISWAHILI, KIINGEREZA, FIZIKIA, KEMIA, BIOLOJIA NA HISABATI, pia panafundishwa somo moja la Chaguo la mwanafunzi kati ya Elimu ya Dini ya Kiislamu ama Maarifa ya Biblia.

Ndugu mzazi/mlezi kamwe usimyime HAKI ya kupata ELIMU kijana wako kwa kisingizio cha UMASIKINI au KIPATO DUNI kwani Elimu ni Ufunguo wa maisha. Aidha kwa kutambua haya serikali ya AWAMU YA TANO inatoa ELIMU BURE kwa kijana wako, Hivyo hauna kisingizio chochote cha kutomleta kijana wako shuleni.

- Shule itafunguliwa JUMATATU ya tarehe **11/01/2021** saa moja kamili na mwisho wa kuripoti ni tarehe 24/01/2021 baada ya tarehe 24/01/2021 ni jukumu la kila mzazi/mlezi kuieleza serikali kwa nini isimchukulie hatua za kisheria kwa kumnyima mtoto wake haki yake ya msingi ya kupata elimu.
    - Iwapo utaona kuna ulazima wa kumpeleka mwanao katika shule za binafsi, itakupasa kumuaga mkurugenzi mtendaji,kwa maandishi, na barua yako ipitie kwa Afisa Elimu Sekondari.

Mwisho, pamoja na barua hii naambatanisha viambata A, B, na C. Mzazi/mlezi yakupasa usome, uelewe na kutekeleza ili kutuondolea usumbufu hapo baadae.

***"Elimu ni Ufunguo wa Maisha"***

***"KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NAMBAMBO"***

**……………….........…….**
**MKUU WA SHULE**

**NAKALA:**

1. Katibu Tawala Mkoa,
   S.L.P 1054
   **LINDI**

2. Mkurugenzi Mtendaji
   Halmashauri ya (W) Nachingwea
   S.L.P 291,
   **NACHINGWEA**

*Kiambatisho "A"*

## 2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### A. SARE ZA SHULE

- **WAVULANA**

(i) Suruali mbili za kushona zenye mfuko mmoja wa nyuma, zenye rinda mbili kila upande wa risani rangi ya damu ya mzee. (Isiwe muundo wa modo, jinzi, akudo ama Ngwasuma)
(ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi
(iii) Viatu jozi mbili vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na soksi nyeupe
(iv) Awe na mkanda wa ngozi au plastiki wa rangi nyeusi

- **WASICHANA**

(i) Sketi mbili ndefu zinazokaribia kifundo cha mguu rangi ya damu ya mzee ndefu kupita magoti mshono wa malinda ya kisu
(ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi
(iii) Viatu jozi mbili vyeusi vya kutumbukiza vya ngozi vyenye visigino vifupi na soksi nyeupe
(iv) Viatu vya shule tunashauri vinunuliwe vya mtumba kwani vinadumu kwa muda mrefu (Bajaji marufuku)
(v) Vazi la Hijabu **(si lazima)** linakamilika kwa kuvaa nguo zilizoainishwa hapa chini na sifa ya kila moja

**1. Sketi**

- Iwe ni yenye urefu hadi kwenye vifundo vya miguu
- Iwe pana na isiwe nyepesi

**2. Blauzi (Nusu kanzu)**

- Iwe ya mikono mirefu isiyofunika viganja vya mikono (iwe pana isibane), Iwe ndefu inayoshuka chini ya makalio (isiwe kama gauni).Isiwe nyepesi

**Muhimu:** Marekebisho ya mavazi ya nguo za kazi kwa wasichana , Bingo na mitandio haviruhusiwi

### B. VIFAA VYA USAFI NA KILIMO

Hakikisha kijana anakuja na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi na kilimo:-
(i) Jembe (Ngwamba) lenye mpini
(ii) Fagio na ndoo
(iii) Fyekeo kwa wasichana
(iv) Panga kwa wavulana

### C. VIFAA VYA MICHEZO

(i) Wavulana fulana ya kijani na viatu vya michezo (raba),
(ii) Wasichana fulana ya rangi ya kijani na viatu (raba)

### D. VIFAA VYA TAALUMA KWA AJILI YAKE

(i) Daftari kubwa (kaunta book quire 2 au quire 3) kumi (10)
(ii) Kamusi ya kiingereza (Dictionary)
(iii) Mkebe wenye vifaa vya hisabati
(iv) Begi ya kubebea daftari (mfuko wa Rambo marufuku)
(v) Ream A4 moja kwa ajili ya matumizi yake binafi, mitihaniya wiki na kazi za nyumbani.
(vi) Shajala (faili kava la karatasi ya khaki) kwa ajili ya kutunzia mitihani yake ya wiki, mwezi na mihula

*Kiambatisho "B"*

## 3.0. 1 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 Aidha, inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais – Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kulipoti shuleni.

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba za shule ni lazima

(iii) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)

(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii

(vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

(viii) Kutunza mali za Umma

(ix) Viduku na unyoaji wa (mitindo hauruhusiwi shuleni)

(x) Bingo na mitandio haviruhusiwi (rejea maelekezo ya uvaaji wa Hijabu)

## 3.0.2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

(i) Wizi
(ii) Uasherati na ushoga
(iii) Ubakaji
(iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli
(v) Kupigana au kupiga
(vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya UMMA
(vii) Kudharau bendera ya Taifa
(viii) Kuwa mjamzito / kupata mimba
(ix) Kuoa au kuolewa
(x) Kutoa mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
(xi) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(xii) Kukataa adhabu kwa makusudi
**(xiii) Kuwa / kukutwa na simu ya mkononi shuleni.**
(xiv) Kufanya kosa litakalodhalilisha jina la shule, uongozi wa shule na Jumuiya ya shule

## 3.0.3. UTAMBULISHO WA MZAZI

Jina la Baba (matatu) ……………………………………..........………(Hai / Amekufa)
Jina la mama (matatu) ……………………………………………......... (Hai/ Amekufa)
Jina la mlezi (kama huna wazazi) majinamatatu ………………………........……
Kitongoji anakoishi Mzazi / Mlezi …………………………………………………............…
Namba ya simu ya Mzazi / Mlezi…………………………………………...……......……..
Jina na namba ya simu ya Mwenyekiti wa kitongoji ……………………….........................…
..............................................................................................................................................

**SAHIHI YA MZAZI / MLEZI …………………………………………….**

*Kiambatisho "C"*

# NAMBAMBO SECONDARY SCHOOL

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**FROM:**
THE HEADMASTER,
NAMBAMBO SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 50,
**NACHINGWEA**

**TO:**
DISTRICT MEDICAL OFFICER
NACHINGWEA GOVERNMENT HOSPITAL,
P.O.BOX 30,
**NACHINGWEA.**

**REF: MEDICAL EXAMINATION**
**(To be completed by Medical Officer)**

I have examined ……………………………………………………………. Who is selected to join in your school as follows:-

| S/NO | AREA | REMARKS |
|---|---|---|
| 1. | Skin | |
| 2. | Eyes | |
| 3. | Ears | |
| 4. | Speech | |
| 5. | Chest | |
| 6. | Spleen | |
| 7. | Abdomen | |
| 8. | Urine | |
| 9. | Stool | |
| 10. | Haemoglobin (Hb) | |
| 11. | Inoculation against meningitis | |
| 12. | Venereal Diseases (VDRL) | |
| 13. | Neurosis | |
| 14. | Any Abnormality | |

I consider that she/he is/his not physically fit to join your school

Name and signature of Doctor ……………………………………………………………

Official Stamp …………………………………………………………………………………….

Date ……………………………………………………………………………………………….

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

## HALMASHAURI YA WILAYA NACHINGWEA

**KAMATI YA WAZAZI,**
SHULE YA SEKONDARI NAMBAMBO,
S.L.P 50
**NACHINGWEA**.

***KUMB. NA. NBB/S 2004/J/*** 14/12/2020

MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………… NA. YA MTIHANI…...........................……

**YAH: KIBALI CHA KUCHANGIA CHAKULA CHA MCHANA NA TAALUMA Na. EA144/249/77/105. KILICHOTOLEWA NA KATIBU TAWALA MKOA WA LINDI KWA SHULE YA SEKONDARI NAMBAMBO**

Husika na kichwa cha habari hapo juu. Kikao cha Kamati ya Wazazi kiliazimia kila mzazi atamchangia mwanafunzi wake kiasi tajwa kama ifuatavyo:-

(a) Mahindi yaliyokubolewa Kg 25 kwa mwaka

(b) Mboga (kunde au Maharage) Kg 12 kwa mwaka

(c) Pesa mahitaji ya mapishi na wapishi Tsh. 15,000/= kwa mwaka.

***Muhimu:***

1. Fedha zote ziingizwe kwa jina la mwanafunzi husika katika akaunti ya wazazi iliyopo **NMB** `namba **70410029292 KAMATI YA WAZAZI NAMBAMBO SEKONDARI,** siku ya kuripoti, fika na karatasi ya Benki ama wakala wa benki ya NMB.
2. Unaombwa kuhudhuria kikao cha kamati ya wazazi na Bodi ya shule kitakachofanyika tarehe 04/01/2021 saa tatu asubuhi ukiwa na mwanao.

Ahsante

**.................................**

**H. PINGILI**

**MWENYEKITI KAMATI YA WAZAZI**